# *Malkia Wa Sheba*

. . .Bwana, naamini,
Mambo yote yanawezekana, Bwana, naamini.

2 Na tuendelee kusimama kwa muda kidogo tu, tutainama kwa ajili ya maombi. Kuna yeyote hapa angetaka kukumbukwa katika maombi mbele za Mungu, kabla. . .tunapowapeleka kwenye Kiti cha Enzi cha neema, sasa? Bwana na akujalie haja yako, tunapoomba.

3 Baba yetu wa Mbinguni, tunakikaribia kiti Chako cha rehema katika Jina litoshelezalo kwa yote la Bwana Yesu, Mwanao. Tunakiri ya kwamba sisi ni dhaifu, Bwana, na tunahitaji msaada Wako, adui yetu mkuu na adui Wako, adui anaenda huku na huku kama simba angurumaye, akimeza awezacho, bali Wewe umeahidi, "Sitawaacha wala sitawapungukia." Nasi tunaamini hilo kwa uchaji sana, Bwana, tukijua ya kwamba "Walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa hapo katikati yao." Nasi tunaamini hilo kwa mioyo yetu yote.

4 Watu wametuma barua, hapa, Baba, na katika barua hizi kuna leso na vipande vya nguo, vinavyowaendea wagonjwa na wahitaji. Na, Ee Baba Mungu, tunafundishwa katika Maandiko ya kwamba walitoa kutoka kwenye mwili wa Mtakatifu Paulo leso ama nguo, pepo wachafu wakawaacha watu, na magonjwa yakaponywa. Sasa, kama tulivyosema hapo awali, tunajua sisi si Mtakatifu Paulo, bali Wewe ungali Yesu, Mwana wa Mungu. Wala hatuamini ya kwamba Paulo ndiye aliyefanya jambo hili, ilikuwa ni Roho Wako, Bwana, akiijibu imani ya watu.

5 Na leo hii kuna haja ile ile, na kilio kile kile, na Wewe ni Mungu yeye yule, jalia matokeo yale yale yaje, kwa kuwa tunawakabidhi Kwako kwa kusudi hilo. Wewe uliiona mikono ya wasikilizaji hawa, Nawe unajua moyo wa kila mmoja, jalia wapokee tu kile walichoomba. Tujalie, Bwana. Tusikie sasa.

6 Na tunapolisoma Neno, tupe Neno kwa Roho Wako Mtakatifu. Ndipo ibada itakapokwisha usiku wa leo, nasi tuanze kwenda kwenye makazi yetu mbalimbali, jalia tuweze kusema kama wale waliokuwa wakitoka Emau, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu?" Fanya jambo fulani usiku wa leo miongoni mwetu, kama tu ulivyofanya kabla ya kule kusulubiwa, ili ulimwengu upate kujua ya kwamba Wewe umefufuka katika wafu, na Wewe si mfu tena, bali Bwana aliye hai milele. Katika Jina la Yesu, tunaomba. Amina.

7 Mnaweza kuketi. Nimekuwa nikiwazia leo, ya kwamba waliita Chicago vibaya kwamba ni Mji wenye Upepo mwingi, nafikiri ilipaswa kuwa ni Tulsa. Ilikuwa vigumu kwangu

kulala jana usiku, upepo ulikuwa mkali sana. Nami nikawazia, “Nimekuwa Chicago mara nyingi, lakini kamwe hakuna upepo kama huo, kama mimi. . . tulivyokuwa nao jana jioni.” Halafu ibada, ilikuwa ngumu sana, upepo ukivuma na kufanya kelele, kidogo ilikuwa ni mchafuko.

8 Lakini yote ililipa leo, kukutana na baadhi ya watu wa thamani. Nilikuwa na majaliwa ya kukutana na Dk. Lamsa, leo, mfasiri wa tafsiri ya Lamsa ya Biblia. Nayo ni majaliwa makubwa mno! Mnajua, afadhali ungenipa tumba dogo la waridi sasa hivi, kuliko shada zima nikiisha kuondoka; nafikiri labda angewazia jambo lile lile. Bila shaka ninaweza kuipendekeza tafsiri yake, kwa kukutana naye na kuona roho ya kupendeza sana ya Mkristo halisi, mwaminio wa kweli. Mungu aibariki nafsi yake shujaa. Sijui kama nimewahi kukutana na mtu mwingine wa kiroho kuliko Dk. Lamsa. Bwana na ambariki kwa wingi.

9 Kisha nilikuwa na majaliwa, leo, ya, katika mahojiano ya faraghani, na kadhalika, kukutana na watu wengine wengi wazuri. Mnao watu wazuri hapa Oklahoma, hakika ninawathamini.

10 Nina u—ujamaa mdogo tu wa Oklahoma, jamani, nafikiri mama yangu aliishi hapa kwa miaka michache, moja kwa moja karibu na Tulsa, hapa. Na kwa hiyo, mimi ni. . . Ndipo wakashuka wakahamia mahali fulani huko Texas panapoitwa Paris, Texas, kisha kutoka hapo, wakaenda Kentucky, wakahamia Indiana, kisha wakarudi Magharibi. Naye baba yangu alikuwa mpanda farasi. Nao mama na baba walikuwa wamefunga ndoa wakati huo.

11 Kwa hiyo basi kwa namna fulani wakahamia Kentucky, kisha wakahama basi, baada ya kuzaliwa kwangu, wakaenda Indiana, na tumekuwa huko tangu wakati huo. Kwa hiyo, ni watu mashuhuri katika Marekani hii, ulimwengu mkuu, watu mashuhuri kila mahali. Mahali unapowapata watu wa Mungu, haidhuru ni wa rangi gani, ama wapi, wanatoka nchi gani, daima ni wale wale.

12 Huko chini sana Ceylon, na sehemu nyingi mbalimbali, ukiwachukua hao watu ambao karibu hawawezi kutofautisha mkono wa kulia na wa kushoto, wanapompokea Roho Mtakatifu, wanatenda kama tu mnavyotenda mnapompokea, bila kujua mkono wa kulia wala wa kushoto, baadhi yao. Nao wanatenda vile vile mnavyotenda mnapompokea Roho Mtakatifu. Kwa hiyo, tunashukuru kwa ajili ya jambo hilo.

13 Sasa hatuna budi kuendelea moja kwa moja, kwa sababu, usiku wa leo, tuliahidi kufanyiza m—mstari mdogo wa maombi kwa ajili ya wagonjwa. Sidai kuwaponya watu, siamini kuna mtu yeyote angefanya hivyo, tunadai tu kwamba tunawaombea.

Ndipo mtu fulani akasema, "Je, wewe ni Mponyaji wa Kiungu, Ndugu Branham?"

14 Nikasema, "La, bwana, mimi si mponyaji wa Kiungu, lakini bila shaka nilikuwa na baadhi ya majibu makuu ya maombi. Kwa hiyo, ninamshukuru Bwana kwa ajili ya jambo hilo."

15 Lakini chochote tunachoweza kufanya kusaidia, baadhi... Kilichonileta hapa, ni kujaribu kuwapunguzia kidogo mizigo ya maisha. Hiyo ni...Kwa namna fulani ni mapambano vyovyote unavyolichukua, sote tunajua hilo. Na kama tunaweza kupunguziana mzigo, kidogo tu, nafikiri inaonyesha upendo halisi wa kindugu na kujaliana.

16 Sasa, ninataka kusoma kutoka kwenye Maandiko usiku wa leo, katika Mathayo Mtakatifu mlango wa 12, kama mtu yeyote anaandika Maandiko, na kifungu cha 42 cha mlango wa 12:

> *Malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa: kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.*

17 Yesu kwa namna fulani alikuwa akiikemea hiyo miji na hao watu, kwa sababu hawakuwa wamemwamini Yeye. Naye alikuwa amewaonyesha kazi zote za Mungu, lakini walikuwa wamekuwa wa kikanisa sana, mpaka wakawa na njia zao wenyewe na mawazo yao wenyewe.

18 Kama vile tu leo, wengi wetu tumejipangia, jinsi tu Bwana atakavyokuja, na wakati mwingine wanajitenga na kuunda dhehebu kutoka kwake, kwa sababu mmoja anaamini Yeye atakuja juu ya farasi mweupe, huyo mwingine juu ya wingu jeupe. Inaleta tofauti gani, mradi tu Yeye anakuja? Hilo ndilo jambo muhimu, iweni tayari. Kwa hiyo, ni—ninaamini ya kwamba atakapokuja, labda itakuwa tofauti kabisa na vile tumewazia, kwa vyovyote vile. Kwa hiyo sina njia yoyote iliyowekwa, ninataka tu kumwona Yeye akija, hivyo tu, na niwe tu tayari atakapofika hapa.

19 Na kwa hiyo, walikuwa wametengeneza njia zao, na theolojia yao ilikuwa imevurugika kidogo, nao walikuwa wamemkana, hata walikuwa wamemwita jina hilo duni la Beelzebuli, ambalo lilikuwa ni mkuu wa pepo.

20 Wakati Yesu alipokuja duniani, alipewa jina duni kuliko yote ambalo lingeweza kutolewa, aliendа kwenye mji ulio duni sana ulioweza kuwako, hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake; ndipo Mungu alipomwinua, alimpandisha juu kuliko Mbingu, mpaka Mbingu, hana budi kuangalia chini apate kuiona. Alimpa Jina lipitalo kila jina, hata kila kitu Mbinguni na duniani kinaitwa Yesu Kristo. Yale Mungu aliyomfanyia, na yale tuliyomfanyia: tulimtendea mabaya, lakini Mungu akamtukuza.

21 Na sasa, Yeye alikuwa akiwaambia jinsi alivyokuwa amefanya, na ile miujiza na ishara alizokuwa amefanya, na kusema, "Kama mambo haya yangalitendeka katika vizazi vingine, mbona, ingalikuwa imesimama bado," ile miji. Na ni ajabu, mwanatheolojia fulani mzuri angeweza kukwambia miji aliyoilaani haipo leo; ile miji aliyoibariki, inadumu hata leo. Ni la kushangaza sana, nami nimewasikia wasomi wazuri sana wa Biblia wakinena habari zake.

22 Lakini Yesu alikuwa amekuja katika kila namna ya Masihi ambaye Biblia ilimbashiri kuja. Alikuwa amekuja kama Mungu-Nabii, Alikuwa amekuja jinsi hasa Biblia ilisema angekuja, na hata hivyo wakakosa kumwona. Loo, jalia huo usiwe ndio msimamo wetu atakapokuja mara ya pili.

23 Sasa, walikuwa wanashindwa kuona kazi Yake ya kimbinguni. Hao watu, makanisa, walikuwa wameenda mbali sana na mambo ya kimbinguni, mpaka wasingeweza kutoa jibu kwa kusanyiko lao kwa ajili ya mambo ya kimbinguni yaliyokuwa yakifanywa, kwa hiyo iliwabidi tu kulibandikia kitu fulani, badala ya kuliwazia, kuweka kando mawazo yao, na—na kwenda kwenye Maandiko, mbona, badala ya kufanya hivyo, walilijibu tu kusanyiko lao, kasema, "Mbona, yeye ni ibilisi, hivyo tu. Yeye ni mpiga ramli tu, ama kitu fulani, hakuna kitu kwake."

24 Lakini basi, wakati alipofanya hayo ya kimbinguni, kwa kawaida huwapofusha wale waliopofushwa wasione mambo hayo, inawafanya wabaya zaidi. Lakini katika kila kizazi, Mungu daima amekuwa na mawakala Wake. Imefikia wakati mwingine akawa ni mmoja tu, bali Mungu daima alikuwa na mtu fulani katika kila kizazi ambaye angeweza kumwekea kidole Chake, baadhi ya watu ambao angeweza kuwawekea kidole Chake, na kusema, "Hawa ni watu Wangu, nao watafanya kama ninavyowaambia wafanye."

25 Naye Yesu alikuwa akirejea nyuma, kifungu cha 41 cha mlango uu huu, Yeye alikuwa amesema juu ya siku za Yona na Ninawi. Watu wengi. . . Ninapenda kuzungumza kwa muda kidogo tu kabla ya kulifikia somo langu, juu ya Yona. Watu wengi sana wanamhukumu nabii huyo. Hapaswi kuhukumiwa, yeye. . . "Ha—hatua za mwenye haki zinaongozwa na Bwana." Naye hufanya kila kitu kitende kazi sawasawa kabisa.

26 Sasa, ninaamini Mungu alikuwa na kusudi katika kumtuma Yona Tarshishi badala ya Ninawi. Ninaamini hilo lilikuwa ndilo kusudi la Mungu la kuwathibitishia Waninawi Neno Lake. Basi wakati Yona, akienda zake Tarshishi, dhoruba kubwa ilitokea, kama tujuavyo, naye akamwambia nahodha wa hiyo meli kwamba alikuwa na hatia. Ndipo wakamfunga mikono na miguu, wakamtupa juu ya—ya ubavu wa meli majini. Maandiko yanasema ya kwamba samaki huyu mashuhuri alimmeza.

27 Kamwe sisahau, wakati fulani uliopita, mtu fulani aliniambia, ambaye alijua mengi kuhusu sayansi akasema, kasema, “Hadithi hiyo haiwezi kuwa kweli, Ndugu Branham.”

Nikasema, “Kwa nini?”

Akasema, “Koo la nyangumi si kubwa kutosha kummeza mtu.”

28 Nikasema, “Lakini bwana, wewe huyasomi Maandiko vizuri, huyu alikuwa ni samaki maalum, aliyeandaliwa. Mungu alimtengeneza huyu vizuri kabisa, Mungu alimwandaa samaki. Akapanua koo lake kusudi Yona aweze kuingia mle. Mungu anaweza kufanya lolote atakalo. Biblia ilisema ya kwamba Mungu alimwekea tayari samaki, na, ambaye angeweza kummeza, alikuwa ni maalum.”

29 Ndipo basi wakati huyo samaki, akizungukazunguka, akitafuta chakula...Basi wakati samaki amekula, kama utawalisha maskini samaki wako wa dhahabu, hebu waangalie, watashuka moja kwa moja chini ya hilo bakuli, na kuzipumzisha maskini pezi zao chini, wakiishakula.

30 Ndipo baada ya, labda, samaki huyu mkubwa kummeza Yona, na akiisha kushuka basi chini ya bahari, nisingejua ingekuwa na kina cha pima ngapi huko nje kutoka Ninawi, lakini hivi ungeweza kuwazia hali aliyokuwa nayo maskini nabii huyu?

31 Mnajua, nafikiri, kama mtu yeyote alikuwa na haki ya kudai dalili, ingekuwa ni Yona. Mwajua, mwangalieni, tunataka kuwazia alikuwa amerudi nyuma, ingawa hakuwa, naye alikuwa kwenye bahari yenye dhoruba katika tumbo la nyangumi, mikono na miguu imefungwa, magugu ya baharini kote kuzunguka kichwa chake, katika matapiko ya nyangumi, amelala chini ya bahari. Sasa, hakuna mtu hapa, aliye mbaya hivyo, nina hakika tu na hilo. Lakini kuonyesha tu ya kwamba huwezi kumficha mwaminio halisi kutoka kwa Mungu.

32 Sasa, ninaweza tu kuwazia kumwona Yona akigeuka mgongoni mwake, basi nena kuhusu kisa kizuri cha dalili: Aliangalia *huku*, ilikuwa ni tumbo la nyangumi, nyuma upande *huu* ilikuwa na tumbo la nyangumi, kila mahali alipoangalia ilikuwa ni tumbo la nyangumi, alikuwa katika hali mbaya sana, dalili nyingi sana. Lakini mnajua yale aliyosema? “Ni ubatili udanganyao.” Akasema, “Mara nyingine tena nitaangalia kuelekea hekalu Lako takatifu, Bwana.”

33 Kwa maana Yona alikumbuka ya kwamba wakati Sulemani alipoliweka wakfu hekalu hilo, aliomba na kusema jambo kama hili katika maombi yake: “Bwana, kama watu Wako wakiwa katika shida mahali popote, kisha watazame kuelekea hekalu hili takatifu, na kuomba, basi sikia kutoka Mbinguni.” Naye Yona alimwamini Mungu, na kuamini maombi ya Sulemani, ndipo Mungu akamwokoa kutoka kwenye tumbo la nyangumi.

34 Sasa, hakuna mtu hapa katika hali hiyo mbaya, hatuko katika tumbo la nyangumi, nasi tuko hapa tukiona mkono wa Mungu ukitenda kazi kila usiku. Na kama Yona angeweza kuweka imani ya namna hiyo, katika hali aliyokuwamo, tumboni mwa nyangumi chini ya bahari, na kukataa kuona chochote kinyume na jibu la maombi yake wakati alipoangalia kwenye hekalu ambamo mtu wa duniani aliombea, na watu wa duniani wakaijenga hiyo hekalu, ni zaidi sana jinsi gani tunavyopaswa kuwa na imani ya kutazama Mbinguni ambako Yesu ameketi mkono wa kuume wa Mungu kufanya maombezi juu ya maungamo yetu? Mbona, bila shaka. Hakuna kitu kinachopaswa kuweza kutuzuia.

35 Yesu, Mwana wa Mungu, aliyesulubiwa, akafa, akafufuka tena siku ya tatu, akapaa Mbinguni, akamtuma tena Roho Mtakatifu anayeshuhudia usiku baada ya usiku, ya kwamba Yeye yupo hapa, basi ni kiasi gani . . .?

36 Tunaendelea kuangalia, tukisema, “Loo, angalia mkono wangu. Angalia kidole changu. Ningali ninaumwa na tumbo.” Loo, jamani, hilo ni baya sana.

37 “Mara nyingine tena nitalitazama hekalu Lako takatifu, Bwana,” ambamo Yeye ameketi mle usiku wa leo, huku amejifunika mavazi Yake yaliyolowa damu, akifanya maombezi tunapokiri.

38 Loo, jinsi ingekuwa . . . Inategemea kile unachoangalia. Kama unaangalia dalili yako, huwezi kupona; bali kataa kuona dalili yako, angalia kile Mungu alichosema. Inategemea kile unachoangalia; naye Mkristo daima huangalia yasiyoonekana.

39 Hivyo ndivyo tu unavyoweza kuokolewa, ni kwa imani, huna budi kuangalia yasiyoonekana. Na silaha zote za Ukristo ni za kimbinguni. Watu . . . Jinsi ambavyo mtu anaweza kusema kwamba anamwamini Mungu, na anahubiri kanisani, na kusema haamini mambo ya kimbinguni, wakati silaha zote za Mungu, silaha kamili za Ukristo, ni za kimbinguni!

40 Silaha za Ukristo ni nini? Upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, upole, subira, imani, Roho Mtakatifu, mambo hayo yote ni ya kimbinguni. Upendo ni nini? Furaha ni nini? Shuka uende kwenye duka la dawa ukaninunulie yenye thamani ya robo, ninaihitaji sasa hivi. Unaona? Huwezi kununua upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, subira, utu wema, imani. Huwezi kuinunua, ni ya kimbinguni. Basi silaha zote za Mkristo ni za kimbinguni, nasi tumeagizwa na Maandiko kuvaa silaha zote za Mungu, tujifunge mshipi, silaha zote.

41 Yona aligeuka katika tumbo hilo la nyangumi, akaangalia upande wa hekalu, vizuri sana alivyojua, kuelekea juu ya nyangumi, na kuanza kuomba. Ndipo Mungu akamgeuza samaki huyo mkubwa, akampeleka moja kwa moja Ninawi kwa kusudi fulani.

42 Sasa, tunaamini ya kwamba wengi wa Waninawi hapana shaka walikuwa wamerudi nyuma, na walikuwa wameenda kombo. . . Nilisoma hadithi wakati mmoja, ambapo wengi wao walikuwa wamegeukia ukafiri, nao walikuwa wakiabudu sanamu, nao waliamini ya kwamba nyangumi alikuwa ni mungu wa bahari. Na wakati kazi yao ilikuwa ni kuvua samaki, huyu hapa nyangumi anakuja akiogelea ufukoni, mungu wa bahari, anafungua kinywa chake na kumtema nabii ukingoni. Si ajabu walimsikia! Mungu anajua jinsi ya kufanya mambo, Yeye anajua jinsi ya kufanya mambo. Ungeweza kuchukua toleo hilo lake ukipenda, hilo huenda likawa ni sawa.

43 Lakini angalieni, jambo muhimu lilikuwa ni hili: kwamba walimwomba Yesu, "Utuonyeshe ishara."

44 Naye Yesu akasema, "Kizazi dhaifu na cha zinaa kinatafuta ishara. Nao watapata ishara." Ishara ya namna gani? Ishara ya ufufuo. Nami ninaamini ya kwamba sasa tunaishi katika wakati wa kizazi dhaifu na kiovu cha wanatheolojia waliochanganyikiwa na makanisa yote yamelundikwa pamoja, hata watu hawajui la kuamini. Lakini Yesu alisema ya kwamba kizazi hicho dhaifu kingepokea ishara ya ufufuo, nami ninaamini tunaipokea sasa. Yesu Kristo hajafa, Yeye yu hai, na yupo hapa usiku wa leo, kuishi ndani yetu, na kutenda, na kufanya yale hasa aliyoahidi atafanya.

45 "Loo," Yeye alisema, "kama Ninawi, kama kizazi hicho kingekuwa kama Ninawi. . ." Kisha anaziendea siku za Sulemani. Naye akasema, "Katika siku za Sulemani. . ."

46 Sasa mtu yeyote anajua, ya kwamba wakati wowote ambapo Mungu anatuma karama duniani, nao watu wanaikataa karama hiyo, daima ni machafuko kwa taifa hilo na watu hao, wanaoikataa karama ya Mungu.

47 Yesu alikuwa ndiye Zawadi kubwa kuliko zote Mungu aliyowahi kuupa ulimwengu. Nao Wayahudi waliikataa, na wakatawanywa kote ulimwenguni tangu wakati huo. Na wakati Mungu anapotuma karama, nao watu wanakataa kuiona, na kukataa kuichukua, basi wanatawanywa, watu wanatawanywa, nao, kama kondoo wasio na mchungaji.

48 Nami nafikiri laiti sisi, usiku wa leo, tungefanya tu kama walivyofanya katika siku za Sulemani! Mungu aliwatumia Israeli karama ya upambanuzi, Naye akaiweka juu ya Sulemani. Basi mara watu walipoona ya kwamba nguvu hizi kuu za Mungu za upambanuzi zilikuwa juu ya Sulemani, waliithamini sana hiyo karama, wakamheshimu huyo mtu, wakamfanya mfalme. Basi msomi yeyote wa Biblia anajua ya kwamba huo ulikuwa ndio wakati wa mafanikio makuu kwa Israeli, siku za Sulemani. Uliitwa wakati wa mafanikio makuu. Israeli walifanikiwa, walijenga hekalu. Hakuna vita hata kidogo, mataifa yote

yaliwaogopa kwa sababu walikuwa wameheshimu kile Mungu alichowatumia.

49 Loo, kama usiku wa leo. . .Mnazungumza juu ya kimbilio dhidi ya bomu, wanajaribu kuchimba futi mia kadhaa chini ya ardhi kupata mahali pa kutengenezea felisi, ili uweze kulikwepa bomu la atomiki. Vema, mtu yeyote anajua ya kwamba bomu hilo lingeipiga dunia na kulipua kina cha futi mia moja, kama ungalikuwa futi mia tano chini yake, ingevunja kila mfupa mwilini mwako. Lakini hakuna kimbilio hapa duniani, ila moja, kuna kimbilio, nalo halijajengwa kwa feleji, limetengenezwa kwa manyoya, chini ya mbawa Zake, ndipo mahali pa kukaa, ndilo kimbilio bora zaidi nijualo, liko chini ya mbawa Zake zinazolinda.

50 Sasa, katika siku za Sulemani, wote walikusanyika, na kuizunguka karama hiyo kuu ya Mungu ambayo ilitumwa kwa Kanisa na kwa watu. Sasa, vipi kama Marekani leo hii, wangeiunga mkono ile Karama waliyotumiwa? Vipi kama tungewafanya Wamarekani wote, ambapo Karama hii kuu imemwagwa katika siku hizi za mwisho, Karama ya Roho Mtakatifu, vipi kama wahudumu wote, walei wote, makanisa yote pamoja, wangekusanyika kumzunguka Roho Mtakatifu, ile Karama ya Mungu, ambayo imetumwa kwetu kutuongoza, na kutuelekeza, na kutuweka katika utaratibu? Lakini tuna maaskofu wengi sana, na maaskofu wakuu, na watu.

51 Mungu anakusudia Roho Mtakatifu kuliongoza Kanisa, huyo ndiye Kiongozi wetu, huyo Ndiye aliyetumwa kwetu, nasi tunapaswa kutawaliwa Naye na Yeye pekee, anayetuelekeza. Ndipo tunadumu katika Neno, sawasawa katika Neno. Roho Mtakatifu huwalisha Chakula cha kondoo, nacho Chakula cha kondoo ni Biblia. Naye humla Roho Mtakatifu. Nafsi inayomwonea Mungu njaa, hula Neno la Mungu. Sasa, laiti sote tungelikusanyika kulizunguka hilo, ni. . .haingetubidi kuchimba futi moja chini ya ardhi, haingetubidi kuogopa shambulizi lolote la atomiki, kwa sababu tayari tungekuwa katika usalama, kusingekuwako na machafuko yoyote miongoni mwetu, sote tungekuwa tukikusanyika huku.

52 Nayo mataifa, Urusi, loo, Urusi ina njaa yake tu kama tulivyo nayo. Na Ufini, wakati mvulana huyo mdogo alipofufuliwa kutoka kwa wafu usiku huo, alikuwa ameuawa katika ajali hiyo ya motokaa, kama nyote mjuavyo, na, katika vitabu imechapishwa, basi huyo mvulana mdogo, nilikuwa nimemwona miaka miwili ama mitatu hapo kabla, katika ono, likaandikwa, niliwaagiza watu waliandike katika Biblia zao, ya kwamba lingetimia, wakati mvulana huyo mdogo alipofufuliwa kutoka kwa wafu alasiri hiyo, usiku huo niliposhuka kwenda Messuhalli, kulikuwako na maelfu ya Warusi wamesimama pale, na hao askari wamesimama pale wakiwa na saluti hizo za Kirusi, machozi yakitiririka mashavuni mwao, kasema, “Tutampokea

Mungu kama huyo." Hakika. Wanakuja kumtafuta Mungu, nanyi mnawapa lundo la kanuni za imani. Wanataka kitu halisi ambacho wanaweza kukishikilia. Siwalaumu.

53 Hiyo ndiyo iliyoanzisha ukomunisti, wakati kanisa lilipoachilia na kuwaacha watu wajilishe kwa mikebe ya takataka. Mtoto mwenye njaa atakula kwenye pipa la takataka, sababu yake pekee ya kufanya hivyo, kwa sababu hajaalikwa kwenye meza safi. Ni kosa la kanisa. Kweli kabisa, ni kosa la kanisa. Mungu hakukusudia kitu kama hicho. Lakini wanaona udhaifu, na si zaidi ya kuwa mwanachama wa chama, wakati unapokuwa mfuasi wa kanisa. Aibu kwetu! Watu wanapokuja kanisani, tunapaswa kuwa na karama zote za kiroho, na nguvu za Mungu zikitenda kazi ambazo zingewafanya watu hao waone kiu.

54 Hivi Yesu hakusema, "Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini chumvi ikipoteza ladha yake, haifai kitu tena, bali kukanyagwa chini ya miguu ya watu"? Hivyo hasa ndivyo walivyofanya nayo. Wakati chumvi ilipopoteza mguso wake wa nguvu, wakati kanisa lilipopoteza nguvu zake, linakuwa si zaidi ya chama kingine chochote. Ni kweli.

55 Lakini chumvi ni ladha kama ikigusana, ikiwa ina nguvu yoyote ndani yake. Kama una nyama *hapa*, na chumvi *hapa*, inakubidi kuzikusanya pamoja, ni sawa kabisa, kuokoa nyama. Ni. . . Chumvi huokoa kama ikigusana, lakini kama chumvi imepoteza nguvu zake, ungeweza kuinyunyizia yote juu ya nyama, nayo ingeharibika, kwa vyovyote vile.

56 Hiyo ndiyo imekuwa shida, watu kujiunga na kanisa, kuandika majina yao kwenye kitabu, pasipo kumjua Kristo kama Mwokozi wao, bila kujazwa na Roho Mtakatifu. Watu wakimwonea Mungu njaa, wakija kanisani, wala hawapati chochote, utupu tu, mazungumzo madogo ya kiakili kuhusu nyota fulani, mwezi, ama kitu kama hicho, ama rais anayefuata ni nani. Mambo hayo ni sawa, bali si mimbarani, mimbara ndiyo kiti cha hukumu, ni mahali ambapo nguvu za Mungu zinapaswa kuhubiriwa katika nguvu Zake na ninii Yake. . . Ni kweli kabisa.

57 Lakini, katika siku za Sulemani, ni tofauti jinsi gani! Wote walikusanyika. Loo, hilo lilikuwa zuri sana! Na wakati wote walipokusanyika kuizunguka karama hii, ilikuwaje? Sifa Zake, na sifa za Mungu zilianza kuenea katika mataifa yote mbalimbali.

58 Sasa, siku hizo hawakuwa na televisheni, na—na telegramu, na—na simu, na kadhalika, njia pekee waliyotuma ujumbe ilikuwa ni kutoka mdomo hadi sikio. Na kila mtu anayepita, Israeli yote, mngeweza tu kuwazia? Moyo wa Israeli ukiwaka moto, wakati mgeni angepita, "Loo, unapaswa kwenda hekaluni. Bwana Mungu wetu ametuma karama, inakaa juu ya Ndugu yetu Sulemani. Mungu amemfanya mfalme mbele zetu, na karama

hiyo iko juu yake. Yakupasa uje uone hekima ya upambanuzi aliyo nayo mtu huyo."

59 Mbona watu wangepitia pale, mioyo yao ingefurahi, wangeenda wamwambie mtu mwingine. Ndipo sifa za Israeli zikaenea ulimwenguni kote mpaka zikafika pande za mwisho za dunia, chini kabisa huko Sheba. Sasa, hiyo wakati huo, nadhani, ilikuwa ndiyo miisho ya dunia, ya ulimwengu uliostaarabika, uliojulikana wakati huo.

60 Kulikuwako na maskini malkia mmoja kule chini, na hebu tuwazie ya kwamba alikuwa ni mpagani. Basi kila wakati msafara wa ngamia ungepita, mtu fulani angekuja, akitoka huko Palestina, hiyo ni kote kote kupitia Jangwa la Sahara, sasa, angeshuka aje mle ndani, na kusema, "Aisee, unajua nini? Unapaswa kwenda Palestina. Hao watu huko juu wana Mungu, wanamwita Yehova, Naye si Mungu aliyekufa, Yeye ni Mungu aliye hai. Yeye si sanamu, mbona, Yeye anaishi moja kwa moja ndani ya mtu aitwaye Sulemani. Mbona, hujawahi kuona kitu kama hicho maishani mwako! Mbona, nguvu zake za upambanuzi ni zaidi ya chochote mwanadamu angeweza kuwazia. Wana kitu ambacho unaweza kushikilia na kusema ya kwamba Mungu wao yu hai."

61 Mnajua, "Imani chanzo chake ni kusikia." Watu wengi sana wakishuhudia, ilifikia mahali ambapo maskini moyo wa malkia huyo ulianza kushangaa. Vema, baada ya kitambo kidogo yeye, akisikia shuhuda nyingi, na imani chanzo chake ni kusikia, hakuna mgongano juu yake hata kidogo, "Unapaswa kwenda uone, ni kweli asilimia mia moja, kila mtu anakuja. Unapaswa kuiangalia, ni karama nzuri sana kutoka kwa Mungu. Nao wana Mungu mkuu."

62 Vema, maskini malkia huyu, hebu na tuliwazie hivi, siku moja aliketi chini na kusoma maandiko yake ya kipagani. Vema, yalikuwa yakiahidi kuhusu mungu mkuu aliyeishi katika sanamu hii, ama *kitu kingine*; naye nyanya alikuwa amejua hilo, na babu alikuwa ameliwazia, na kadhalika. Lakini baada ya kitambo kidogo alikuja kusikia shuhuda hizi, haikuwa ni theolojia fulani iliyoandikwa, ilikuwa ni uhalisi ulio hai.

63 Nami nitawaambia, kama. . .hakuna mtu ulimwenguni aliyewahi kutoka nyuma ya pazia akaingia ndani ya nuru hii tunamoishi, inayoitwa maisha, ila ambaye anashangaa anaenda wapi anapoenda ng'ambo ya hapa. Ni silika tu ndani ya mwanadamu kufanya hivyo. Sisi sote tunatafuta, tunataka kujua kuna nini ng'ambo ya pazia, tunatafuta kujua hayo.

64 Maskini huyo malkia akaanza kuona njaa, akawazia, "Loo, kama mimi. . .ninaamini nitaenda. Na baada ya kitambo kidogo akaamua, "Ninachoka kuwasikiliza wengine wakiniambia kuhusu hilo, sijui kama ni kweli ama si kweli, bali ninaenda

kujionea mwenyewe." Hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo. Nenda, ukajionee mwenyewe, usisimame nyumbani na kukosoa.

65 Wakati Filipo alipomwona Nathanaeli alisema, "Njoo, umwone Yule tuliyemwona, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu."

Akasema, "Sasa, laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?"

66 Akasema, "Njoo, uone." Hilo ndilo jambo bora kuliko yote la kujishawishi. "Njoo, uone." Filipo alimpa Nathanaeli jibu zuri kuliko yote ambalo mtu yeyote angeweza kutoa, "Njoo, ushawishike mwenyewe."

67 Vema, maskini mwanamke huyo aliwazia angeenda na kushawishika kama ilikuwa ni kweli ama si kweli. Lakini sasa, alikuwa na mambo mengi ya kumkabili, mengi zaidi kuliko tuliyo nayo mimi na wewe, kujaribu kupata ukweli.

68 Jambo la kwanza, kabla hajaondoka, alikuwa ni malkia, naye alikuwa na mamlaka makubwa, na hapana shaka ya kwamba jina lake kwenye kile kitabu kikuu cha kanisa pale, lilikuwa na uzito sana, kwa hiyo jambo la kwanza analopaswa kufanya, lingekuwa ni kwenda kuzungumza na kasisi wake mpagani, na kumwomba ruhusa kama angeweza kuondoka kanisani na kwenda huko na kutafuta kujua kuhusu dini hii nyingine.

69 Mbona, ungeweza tu kuwazia alipata jibu la namna gani. Mbona, ninaweza tu kumwona kasisi huyo mpagani, mwajua, akisimama pale, na kusema, "Sasa, ngoja kidogo, binti, unajua, hutaki kufuata falsafa za bure namna hiyo, kwa sababu nawaambia, kama kungekuwako na mungu yeyote aliye hai, ingekuwa ni mungu wetu."

70 Unajua, huenda tusiwe na makafiri, bali tuna makasisi wa aina ile ile, vema. Naam, bwana. "Kama Mungu angefanya jambo lolote la kimbinguni, angelifanya hapa kanisani mwetu. Asingeenda kule na kufanya hivyo, angelifanyia hapa." Lakini, mnajua, jambo ni kwamba, Mungu hulifanyia mahali anapotaka, na jinsi anavyotaka, na si juu yetu kumhoji Mungu.

71 Ndipo tunaona, ninaweza kumwona kasisi akisema, "Sasa, angalia, binti, nyanya yako, nyanya wa nyanya yako, na huko nyuma yake, wote waliabudu sanamu hii kuu hapa, ni mungu mkuu."

72 Akasema, "Naam, bwana, hiyo labda ni kweli. Nina magombo yote juu yake, lakini nimesikia gombo hili lote, na tena, na tena, na tena, kile ambacho angefanya, kile ambacho angefanya, bali sijamwona akipiga hatua hata moja." Hilo ni jibu zuri. "Sijaona jambo moja. Yote ninayoona ni kipande cha jiwe kilichowekwa pale."

73 Na kama hayo tu ndiyo uliyo nayo, ndugu, wewe ni kama tu, karibu katika hali mbaya kama yeye alivyokuwa. Hiyo ni

kweli. Kipande kikubwa cha jiwe la jengo, ama *kitu kingine*, kinachoitwa, “Hili ni kanisa langu, hili ni dhehebu langu.” Hayo yote ni sawa, lakini hayo siyo ninayozungumzia, ninazungumza juu ya Mungu aliye hai, Yule ambaye hajafa, Yule aliye hai sasa hivi, Yule aliye hapa, halisi tu kama alivyowahi kuwa halisi. Aliahidi hilo.

74 Halafu basi, anasema, “Mbona, angalia, bwana, sijawahi kumwona akisogea, sijawahi kumwona akifanya lolote, nyanya yangu hakuwahi kumwona akifanya lolote, na wala mama yake hakuona. Nami nimeishi mpaka wakati huu, nami nasikia ya kwamba kuna Mmoja aliye hai, ninaenda kumwona. Haidhuru unawazia nini, ninaenda, kwa vyovyote vile.” Ninapenda ujasiri huo. Jionee mwenyewe. Akasema, “Sasa, kama si sahihi, nitarudi na kukwambia si sahihi, bali nitajua moyoni mwangu kama ni kweli ama si kweli.”

75 Sasa, ninaweza kuwazia kabla hajaanza, kwamba alikuwa na mawazo fulani niani mwake namna hii: “Vipi kama si kweli? Ama vipi kama ni kweli? Sasa, kama ni kweli, na kuna Mungu aliye hai, anayetenda kazi, yu hai miongoni mwa watu, na kujionyesha Mwenyewe kuwa hai, si jiwe, bali Mungu aliye hai, kama ndivyo, nitaliunga mkono kwa kila kitu nilicho nacho, kinastahili.”

76 Akatandika ngamia wake, na—na kuchukua shehena kubwa ya fedha, dhahabu, manemane, uvumba, yuko tayari kuanza. Sasa, huenda aliwazia hivi: “Kama ni kweli, nitaiunga mkono. Lakini kama si kweli, nitarudisha pesa zangu nyumbani.”

77 Hilo ni wazo zuri kwa Marekani. Labda sikupaswa kusema hivyo. Nitangojea tu kwa dakika moja, niache lizame ndani kabisa. Kama ni Mungu, liunge mkono kwa maombi, kwa yote uliyo nayo. Fanya kila uwezacho kulieneza, sio sana kwa pesa, pesa kidogo mara kwa mara hulisaidia, bila shaka, lakini, zinapohitajika, saidia, lakini jambo muhimu ni kuweka pesa mbali sana nalo uwezavyo, jiweke mwenyewe humo ndani badala ya pesa zako. Mungu anakutaka wewe madhabahuni, si pesa zako. Ni afadhali kwako ku. . . Na hili. . . mimi. . .

78 Pasaka hii inayokuja daima inanifanya kidogo niwe nusu, mgonjwa kiroho, ulaji wangu wa kiroho hauwezi kuyeyusha hayo wanapopanda juu na kuweka chungu kikubwa cha yungiyungi madhabahuni. Mungu hataki mayungiyungi madhabahuni, anakutaka wewe madhabahuni, madhabahu hazikujengwa kwa ajili ya mayungiyungi. Kaini aliwazia hivyo, nanyi mnaona kilichotukia. Madhabahu ilijengwa kwa ajili yako, wewe ndiye kafara inayopaswa kuwa madhabahuni.

79 Basi akasema, “Kama sivyo, nitarudi na pesa zangu.” Sasa, alipowaweka ngamia wake wote tayari. . . Na bila shaka hakuna hata mmoja wa watu hao kule chini aliyetaka kwenda, labda. Pia kumbukeni, alikuwa na safari ndefu, na ilimbidi kuvuka

Jangwa la Sahara, naye hakuwa na Kadilaki iliyoyoyozwa, alikuwa na ngamia wa kumpanda, na huo mchanga wenye joto, unaochemka.

80 Si ajabu Yesu alisema, "Atasimama katika Siku ya Hukumu na kukihukumu kizazi hiki kuwa kimekosa." Alikuja moja kwa moja kupitia hilo jangwa, ikamchukua miezi mitatu kufanya hivyo, huku watu wengine hawatavuka barabara kwa dakika tatu kuona madhihirisho ya Mungu aliye hai, akiishi miongoni mwa watu Wake, lakini watawahesabu kama kundi la watakatifu wanaojibingirisha . . . ? . . . Si ajabu taifa hili linastahili hukumu.

81 Huko, ilimbidi kuvuka jangwa hilo. Pia kumbukeni, wana wa Ishmaeli walikuwa jangwani siku hiyo, hao wapanda farasi na wanyang'anyi wakuu. Ni mawindo rahisi jinsi gani kwa lile jeshi dogo alilokuwa nalo, na wasichana wachache, maskini huyo mama ameketi juu ya ngamia. Labda ilimbidi kusafiri usiku, mi—miale ya moja kwa moja ya jua hilo karibu ingemwunguza, mchana. Wakichunguza na kuona kama wangeweza kufuata nyota usiku iwaongoze kwenye shimo fulani la maji huko Sahara, wakivuka. Loo, alikuwa na mambo mengi ya kuwazia.

82 Lakini sikilizeni, hebu niseme hivi: Mungu anaponena katika moyo wa mwanadamu na kuanza kuwavuta, hakuna pepo wa kutosha kutoka kuzimu kuwazuia wasiliendee, wataliendea. "Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu." Kitu fulani kinaanza kuchimba katika moyo wa mwanadamu. "Kuna Mungu mahali fulani, Ninamtafuta." Atatafuta, na kusogea, na kuwinda, na kugeuza mpaka ampate.

83 Na kama Daudi alivyosema katika siku zilizopita, "Kilindi kinapoita kilindi." Kama kuna kilindi kinachoita, hapana budi pawe na kilindi cha kukiitikia. Sikilizeni, kama hakuna Maandiko yanayoniambia ya kwamba kulikuwa na uponyaji wa Kiungu, ninyi watu mnaoketi hapa usiku wa leo, ningali ningeamini ya kwamba kulikuwako. Angalieni, kabla hapajawa na ki—kiumbe, hapana budi kuwe na Muumba kuumba hicho kiumbe.

84 Labda hicho ni Kiyunani kwenu, lakini sikilizeni, hapa—hapa wakati fulani uliopita, nilisoma kwenye gazeti, mji mmoja chini yetu, ambapo mvulana mdogo alikuwa akila vifutio kutoka kwa penseli, naye mwalimu alifadhaika sana juu yake na akatuma habari kwa mama yake. Huyo Mama akamwona maskini jamaa huyo nje barazani, akila pedali ya baiskeli, mpira. Kwa hiyo akampeleka kwenye kliniki, nao wakamchunguza maskini jamaa huyo, nao wakakuta kwamba maskini mwili wake ulihitaji salfa, nayo salfa ilikuwa katika mpira. Lakini kabla hajaweza kutamani salfa, ilibidi kuwe na namna fulani ya salfa huko nje kuitikia shauku hiyo, la sivyo asingeitamani kamwe.

85 Na mradi tu wanadamu wanatafuta, na kuona njaa, na kuona kiu, wakiziitia nguvu za Mungu, hapana budi pawe na nguvu za Mungu mahali fulani kuiitikia. Kabla hapajakuwapo na kiumbe, hapana budi kuwe na Muumba mle ndani akiumba hicho kiumbe.

86 Mtu anapotamani kumwona Mungu, hapana budi pawe na Mungu mahali fulani aliyeumba hiyo shauku ndani yake. Kama kilindi kinaita kilindi, hapana budi pawe na kilindi cha kuitikia hicho, kwa sababu ilibidi kilindi kiwepo kwanza kipate kuumba wito huo ulio ndani yako.

87 Sasa, maskini mwanamke huyo alikuwa akienda zake, kila kitu dhidi yake. Lakini mara, alipopata hisia ya kwamba Mungu alikuwa ni Mungu halisi, Mungu alikuwa halisi, akaanza kuona kiu. Mwingine akaingia, akasema, "Loo, nilimwona akisimama . . . Moja ya mambo ya ajabu sana niliyopata kuona, bali alilitatua moja kwa moja chini ya nguvu za Mungu wake, na kuwapa jibu kamili." Loo, ilimtikisa tu maskini malkia huyo.

88 Akasema, "Loo, lazima niione! Lazima niione! Mimi ni mwanadamu, maisha yangu, kikomo changu cha Milele kiko mbele yangu, lazima niione." Hakuna kitu kilichokuwa kinaenda kumzuia. Huwazii hatari, huwazii kukosolewa, huwazii yale mtu mwingine atakayosema.

89 Wakati Malaika yule wa Bwana alipokutana nami huko juu usiku huo . . . Ndugu zangu wote kanisani mwangu waliniambia, kasema, "Hayo maono ni, huyo ni ibilisi. Wewe—wewe ni mwana mizimu." Lakini wakati . . . Kamwe nisingeweza kuona ni kwa nini ingewezekana, nami nikimpenda jinsi nilivyompenda. Nilipokutana na Yeye huko juu usiku huo, loo ndugu, kilindi kilikuwa kikiita kilindi, na kulikuwa na Kitu fulani kilichokiitikia.

90 Nilimwendea mwangalizi wa kanisa, akasema, "Billy, ulikuwa na jinamizi."

Nikasema, "Kama hivyo—kama hivyo ndivyo kanisa hili linavyojisikia kulihusu, hii hapa kadi yangu ya ushirika."

Kasema, "Loo, sikulimaanisha hivyo. Lakini, unajua, *ninii* haiwezi kutukia."

91 Nikasema, "Vema. Afadhali niache ushirika sasa, maana mtanifukuza baada ya kitambo kidogo, kwa vyovyote vile. Kwa hiyo afadhali nianze huru na safi na nishike mwendo." Kwa hiyo hilo hapo. Wakati kilindi kilipokuwa kikiita, kuna kitu cha kukiitikia.

92 Sasa, baadhi yao walisema, "Huyu Goliathi mkubwa mno hapa nje, sayansi ya tiba, na makanisa haya yote mazuri, yaliyostaarabika . . . "

93 Nikasema, "Siwezi kujiepusha na jinsi gani alivyo Goliathi, Mungu angali ni Mungu. Mungu wa Daudi angali anaishi,

Mungu wa Ibrahimu angali anaishi, Mungu wa Yakobo anaishi, Mungu aliyekuwa ndani ya Kristo anaishi usiku wa leo, amefufuka, nami ninajua Yeye ni halisi."

94 Kuna kitu ambacho, haidhuru shida ni nini, unataka kwenda, kwa vyovyote vile, kwa sababu kuna...una lengo. Na kama utachukua nia nzuri ya lengo hilo, utafika. Huna budi kuwa na nia nzuri kwa lengo lako. Hivyo ndivyo daima ninavyopata mapenzi ya Mungu, kwanza, nawazia kama ni mapenzi ya Mungu, halafu lengo langu na kusudi langu kwake. Kama ni lengo zuri, basi kusudi, nililo nalo.

95 Kama Mungu angesema, "Nenda hapa ukahubiri kwenye kundi *hili*."

96 Ningesema, "Vema, nitapata kiasi gani katika sa—sadaka ya upendo?" Bila shaka hilo limeamuliwa kabisa, ninapata dola mia moja kwa juma haidhuru kama nikihubiri au la. Hilo latosha. Kwa hiyo, lakini hata kabla ya hapo, kabla sijapata mshahara, haileti tofauti yoyote ilikuwa ni wapi, kusudi sahihi ni kuona kile ungeweza kufanya kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Nenda mahali anapokuongoza kwenda, haidhuru ni wapi, kama ni ndogo au pungufu.

97 Kamwe sijaruhusu mikutano yangu kukua ama kupata ukubwa wowote. Sihitaji pesa nyingi, nina taipureta mbili kwenye sehemu moja ndogo pembeni mwa trela, wavulana wawili ninaowalipa, hivyo tu. Kwa nini? Huenda Mungu akaniita mahali padogo *hapa*.

98 Hivi majuzi tu nilifanya uamsho katika kanisa lililokuwa na watu ishirini. Halafu, kama akinitaka niende ng'ambo na kuwahubiria laki moja, ama laki mbili, chochote kile, Yeye huliweka juu ya moyo wa mtu fulani kunituma kule wakati ule ule anaponipa wito. Loo, hakuna kitu kama hicho! Namwishia, namtumainia siku baada ya siku, aongoze, mahali kilindi kinapoita.

99 Maskini mwanamke huyo akasema, "Ninaenda, kwa vyovyote vile." Huyo akavuka hilo jangwa, bila kujali lolote la mambo ambayo watu walisema, haidhuru, akakaza mwendo.

100 Vema, hatimaye akawasili langoni. Ninaweza kumwona akipakua mizigo yote kutoka kwa ngamia, na kuweka dhahabu ndani ya hema. Na sasa, yeye hakuja kusema tu, "Nitaingia, nilisikia habari za mwinjilisti huyu, nitaingia na kuketi chini, lakini kama akisema jambo moja dhidi ya fundisho la kanisa langu, nitasimama mara moja nitoke."

101 Hilo ni toleo lake la 1960, watu walijua vema zaidi katika siku hiyo. Nafikiri kwanza kabisa hilo linaonyesha malezi duni. Hiyo ni kweli. "Kama ni kitu chochote kinyume changu, kama akisema neno moja, nitasimama mara moja nitoke nje, sitamsikiliza tena. La, bwana. Sitamsikiliza."

102 Unaona, huji kwa nia nzuri, huji kwa lengo sahihi la kujaribu kumtafuta Mungu, unajaribu tu kuyavuruga kabisa maarifa yako, huna njaa ya Mungu bado. Ukiwa na njaa ya Mungu, utakaa mpaka itakapokwisha, kama alivyofanya.

103 Alipiga hema lake na kadhalika, kisha akajiandaa na kupiga kambi huko nje uani mwa ikulu mahali fulani, na kusema, "Nitakaa hapa mpaka nitakapoyaona yote. Kama ni kweli, ni kweli; kama ni uongo, ni uongo."

104 Kwa hiyo ninaweza kuwazia nikimwona akishuka kwenda Yerusalemu na kununua magombo yote ya Kiebrania yaliyokuwepo, wapate kujua Mungu huyu alikuwa wa aina gani waliyekuwa wakinena habari zake. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

105 ". . .mnadhani mna Uzima wa Milele, Nayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Kama mambo unayoona yakifanywa si ya Kimaandiko, basi usiyaamini.

106 Hivyo ndivyo alivyokuwa anaenda kufanya, kuchukua Gombo, na kusema, "Sasa hebu tuone huyu Yehova ni Mungu wa aina gani." Naye akasoma kabisa, akasema, "Ninajua tu kile Yeye atakachokuwa sasa."

107 Sasa, kama tu ungefanya hivyo, kama watu wa Marekani wangekuwa tu na welekevu kama huo, kama wangekuwa tu kabisa na. . .wamtafakari Mungu kiasi hi—hicho! "Je, Yeye aliahidi kufanya jambo hili? Ni mapenzi Yake? Je, Yeye aliahidi atafanya hivyo? Ni Roho Mtakatifu? Ni asili gani? Inatendaje kazi?" Hivyo ndivyo unavyopaswa kufanya. Tafuta kujua kama Roho Mtakatifu ni. . .

108 Unaenda kule na kusema, "Ni—ninamwamini Mungu Mwenyezi, ninaamini Yesu ni Mwanawe. Ninachukua. . ." na kupewa kipaimara? Kamwe hapajakuwako na kitu kama hicho. Hupewi kipaimara, ni kuzaliwa kwa Roho Mtakatifu, kuzaliwa kwa Roho.

109 Angalia kama jambo hilo ni sawa. Lichunguze tena, uone kama unatakiwa kunyunyiziwa, ama kubatizwa kwa kuzamishwa. Angalia kama unapaswa kujiunga na kanisa, ama kuwa, ama, kumpokea Roho Mtakatifu. Nimekuwa pamoja na familia ya Branham, Jumatano ijayo, miaka hamsini na mmoja, kamwe hawakuniomba nijiunge na familia hiyo, nilizaliwa Branham, hiyo ndiyo sababu. Na, mimi—mimi. . .Unazaliwa katika Kanisa la Mungu aliye hai. Ni tukio. Unakuwa kiumbe kipya, wewe ni mtoto wa Mungu, mwana wa Mungu.

110 Na kama Roho wa Mungu anakaa ndani yako, atashuhudia pamoja na Neno Lake Mwenyewe. Mtu akisema, "Vema, hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya siku nyingine." Kumbuka, huna Roho wa Mungu ndani yako. Kama Biblia ilisema, "Yesu Kristo, yeye yule jana na hata milele," unasema, "Kwa njia fulani." Basi kumbuka, huyo ni ibilisi ndani yako. Hiyo ni kweli. Si

Mungu. Mungu asema, “Naam, bwana, kila Neno, hilo ni amina. Amina, nililiandika. Amina.” Watu wa kale, walipoongozwa na Roho Mtakatifu, waliandika Biblia. Roho Mtakatifu anawezaje kuikana?

111 Siwapigii kelele. Nimezoea kuhubiri huko nje, kwa hiyo, ninaninii . . . Ninajua hamna uzito wa kusikia, lakini mimi—mimi si . . . Ninajisikia tu kubarikiwa, hivyo tu, nina—ninajisikia tu vizuri sana. Ni Roho Mtakatifu, maana ninajua jambo ninalozungumzia ni kweli, ni kweli ya Mungu.

112 Maskini mwanamke huyo alisogea huko juu. Nami ninaweza kumwazia, nikiona siku ya kwanza, akichana nywele zake upesi sana, na kunawa uso wake, na kufika kule, akasema, “Nitaona kile kusanyiko lote . . . ” Hawa hapa watu kutoka kila mahali, wamekusanyika kwenye nyua kubwa. Na baada ya kitambo kidogo, baada ya wao kuimba baadhi ya Zaburi, ninaweza kumwona Mchungaji Sulemani akitokea, akija, akaenda kwenye kiti chake, akaketi kwenye kiti chake cha enzi.

113 Basi jambo la kwanza, hiki hapa kisa kinatokea. Na mara kilipotokea, alisema, “Sasa, nitaona tu kuhusu hili na kuona jinsi hili linavyofanya kazi, nilisikia kulikuwa na hekima nyingi sana. Sasa mwangalie maskini huyo mwanamke, ama yeyote yule, amesimama pale, tutalishughulikia.”

114 Alipofika kwa Sulemani, alimwambia jambo lililo sahihi kabisa. Maskini moyo wake ukaanza kudunda, “Jamani, hilo halina budi kuwa ni kweli. Hebu tuone haya Magombo, sawa kabisa, hiyo haina budi kuwa ni kweli.”

115 Siku baada ya siku ikapita, akaketi, angeingia ndani, labda usiku, aketi kando ya nuru ya mshumaa, asome, asome, asome Maandiko, asome Isaya, asome manabii wote, akijiandaa, akishangaa ni kitu gani hasa kitakachotukia. Arudi kesho yake, na kuona Mungu yeye yule aliyekuwa amesoma habari Zake, akiishi katika mmoja wa viumbe Vyake vya kibinadamu, vinavyopatikana na mauti, akijitangaza Mwenyewe kupitia mtu huyo. Mtu huyo, aliyejisalimisha sana kwa Mungu, hata Mungu akafanya kazi kupitia kwake. Si mtu huyo, mtu huyo alikuwa ni mwanadamu tu, kama wewe au mimi.

116 Hili si Kanisa siku hizi. Si ninii . . . Petro aliuita Mlima wa Kugeuka Sura, wakati mmoja, “mlima mtakatifu.” Siamini huyo mtume alimaanisha mlima mtakatifu, maana huo mlima haukuwa mtakatifu, Ilikuwa ni Mungu Mtakatifu juu ya mlima. Si Kanisa takatifu, ni Roho Mtakatifu Kanisani anayelifanya takatifu. Si watu watakatifu, mtu mtakatifu, hakuna kitu kama mtu mtakatifu, kanisa takatifu, ama *hili* takatifu, ama *lile*, ni Roho Mtakatifu Kanisani, ndani ya watu, Mungu Mtakatifu, akijiendesha Mwenyewe kupitia kwa watu. Jambo ndilo hilo.

117 Chemchemi, Chemchemi ya Uzima isiyokwisha ni Kristo. Huwezi kuumaliza upendo Wake mkuu, na nguvu, na nia ya

kukushughulikia. Wema Wake na rehema, zimepita ufahamu wa kibinadamu. Tunalala tu mle ndani na kuogea humo, hivyo tu, katika rehema Zake.

118 Ndipo akachunguza, siku baada ya siku. Hatimaye, ikafika wakati ambapo kadi yake ya maombi iliitwa, ama chochote kile, huenda haikuwa kadi ya maombi, bali chochote kile, wakati wake wa kuja mbele zake ukafika. "Sasa," akasema, "Nina mambo fulani . . . " Lakini Biblia ilisema ya kwamba hakuna kitu alichofichwa Sulemani, pasipo yeye kujua habari zake. Amina. Hakuna kilichofichika, alimwambia mambo yote. Kama hiyo . . .

119 Hiyo ilikuwa ni Roho ya namna gani juu ya Sulemani? Sulemani? La, bwana. Ilikuwa ni Roho ile ile iliyonena na mwanamke kisimani na kumwambia ambapo ninii yake . . . kwa nini alikuwa akiishi katika uzinzi. Naye akaenda na—na kuwaambia watu, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo yote niliyofanya!" Alijua kama Yeye angeweza kumwambia jambo hilo moja, Yeye angeweza kumwambia mambo yote. Wala hakuna kitu kilichofichika ambacho Sulemani hakumwambia.

120 Yeye alisema nini? Mnajua alifanya nini? Alisimama hadharani, mbele ya kusanyiko la watu, naye akasema, "Yote niliyosikia kukuhusu wewe, mambo yote mazuri niliyokuwa nimesikia kukuhusu, yalikuwa kweli, na zaidi ya yale niliyopata kusikia kukuhusu." Yeye mwenyewe alipata hilo tukio.

121 Na kama huamini kwamba Roho Mtakatifu ni halisi, yale uliyosikia juu Yake, wewe pata tu hilo tukio mwenyewe uone kinachotukia. Angalia kama hutasema, "Zaidi ya yale . . . "

122 Nilizoea kuwaangalia watu wakifurahia baraka za Mungu, nilifikiri ilikuwa ni sawa, kwa hiyo nilitaka jambo hilo. Lakini utakapoipata, basi utasema, "Ni zaidi ya yale niliyowahi kuona," kwa sababu ni jambo lililokufanyikia *wewe*, wakati Kristo anapojifunua Mwenyewe kwako, si katika hali ya kiakili, bali katika kuzaliwa upya.

123 Alisimama pale, isitoshe, alitambua ya kwamba mtu huyo alikuwa na Mungu ndani yake, na hiyo ilikuwa ni karama ya Mungu, akasema, "Yote niliyosikia ni kweli, na hata zaidi ya niliyosikia." Naye akasema, "Hata wamebarikiwa watu walio pamoja nawe, heri watu wanaoketi hapa pamoja nawe kila siku, wanaoona karama hii kuu ya Mungu ikitenda kazi. Heri watu walio pamoja nawe, wanaosimama . . . "

124 Sasa, wazia juu ya mpagani akisema hivyo. Alishuhudia ya kwamba Huyo alikuwa ndiye Mungu wa kweli. Naye Yesu alisema, "Atasimama katika Siku ya Hukumu, naye atawahukumu watu wa kizazi hiki kuwa wamekosa," ambao hawatavuka barabara, ama waingie na kuketi chini, waangalie pande zote kidogo, na kusema, "Loo, hilo ni bure," waondoke.

125 Katika Siku ya Hukumu, kama atawahukumu watu wa kizazi hicho, vizazi vichache tu baada ya Sulemani, naye Yesu

alisema, "Aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa," na ni mkuu sasa kuliko vile ilivyokuwa wakati Yesu alipokuwa hapa, kwa kuwa walimwambia ya kwamba Yeye alikuwa ni Beelzebuli, wakayaita matendo ya Roho wa Mungu mwanamizimu, ama kitu fulani, na kumwita Yeye Beelzebuli, kwa sababu Yeye alifanya hivyo, naye Yesu akasema, "Nitawasamehe, lakini Roho Mtakatifu atakapokuja, kunena neno dhidi Yake, hakutasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao," kwa hiyo Moja ya zawadi kuu sana ambazo Mungu amewahi kutoa ilikuwa ni Mwanawe, kuwatakasa watu kusudi Roho Mtakatifu aweze kujionyesha Mwenyewe, na hata hivyo, maskini mwanamke huyo, kama angehukumu hilo, hii ni miaka elfu mbili baadaye, atafanya nini atakaposimama mbele ya Tulsa, kwenye Siku hiyo?

126 Atafanyaje, wakati atakaposimama mbele ya Marekani yote katika kizazi hiki? Yeye ataihukumu, kwa kuwa hakuwa na kikomo. Moyo wake ulikuwa na njaa naye akaitambua, alimtafuta Mungu, akayachunguza Magombo, akaona ilikuwa sahihi, ndipo akakubali, na kusimama na kumbariki, akawabariki hao watu, naye alifurahi sana kwamba alikuja.

127 Nina furaha sana, kwamba siku moja niliona kwamba ni kweli. Loo, imekuwa:

> Wewe, Kijito cha faraja yangu yote,
> Zaidi ya maisha kwangu,
> Ni nani niliye naye duniani mbali na Wewe?
> Au ni nani Mbinguni ila Wewe.

128 Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Hebu na tumkumbatie Yeye, Zawadi ya kweli ya Mungu, Mwana wa Mungu katika umbo la Roho Mtakatifu.

129 Na tuinamishe vichwa vyetu. Kabla ya kuomba, huku vichwa vyenu vimeinamishwa na macho yenu yamefumbwa, ni wangapi wangetaka kukumbukwa katika maombi usiku wa leo, wakisema, "Ndugu Branham, nikumbuke mbele za Mungu. Ninatambua ya kwamba Roho Mtakatifu yuko humu duniani leo, ya kwamba nguvu kuu za Mungu zingali zinatenda kazi kupitia kwa waaminio kama Yesu alivyoahidi, 'Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya. Yeye aniaminiye Mimi,'" Yohana Mtakatifu 14, "yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya"?

130 Alijitambulishaje kuwa Masihi? Kwa kujua siri za mioyo yao. Hiyo daima imekuwa ndiyo ishara ya Mungu kote katika wakati. Je, mngependa kukumbukwa? Inueni mikono yenu. Mungu awabariki, kila mahali.

131 Kama vile Wewe ulivyosema katika Neno Lako, Bwana, "Heri macho yanayoweza kuona, na masikio yanayoweza kusikia." Na kwa kweli, hakuna mtu awezaye kuja, usipomvuta. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya Roho Mtakatifu.

Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya watu hawa walio hapa usiku wa leo, ambao wamempokea Roho Mtakatifu. Tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba wote hapa ambao hawajampokea, watampokea usiku wa leo. Isafishe mioyo yao kutokana na kutokuamini, na jalia waamini tu, kwa imani rahisi kama ya kitoto, wakikiri, ifungue mioyo yao, Naye hakika atakuja kwenye makao ya—yao. Tujalie, Bwana.

132 Ibada zinakaribia sasa, Bwana, kwenye mstari wa maombi, ambapo mtumishi Wako, nitawaombea wagonjwa ikiwa ni mapenzi Yako. Ninaomba, Bwana, ya kwamba kama kuna wenye dhambi hapa, wasioamini, loo, huenda ni wanatheolojia, huenda wakawa washiriki waaminifu wa kanisa, lakini kama bado hawajampokea Roho Mtakatifu, ama kumwamini Yeye, wangali ni wasioamini.

133 Kwa kweli, Bwana, Ibrahimu alimwamini Mungu, na ikahesabiwa kwake kwamba ana haki, ndipo basi Mungu akampa muhuri wa tohara kama thibitisho la imani yake. Ndivyo ilivyo leo, Bwana. Huenda tukasema tunaamini, lakini mpaka tutakapompokea Roho Mtakatifu, haijathibitishwa kamwe, kwa maana imeandikwa katika Kitabu cha Waefeso, mlango wa 4 na kifungu cha 30, “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri hata Siku ya ukombozi wenu.” Jalia iwe ni usiku wa leo, Bwana, kwamba Wewe utawatia wengi muhuri uwaingize katika Ufalme wa Mungu, mpaka Siku ya ukombozi, jalia wawe waaminio kamili usiku wa leo, Nawe ulithibitishe kwa kuwapa Roho Mtakatifu.

134 Ee Bwana, ningekuomba Wewe, Mungu, jalia aje sasa na kuinyenyekeza tu mioyo yetu, na kutuleta mahali ambapo angeweza kufanya kazi kupitia sisi na ndani yetu kuonyesha mapenzi Yake, na kufanya mapenzi Yake. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

[Dada mmoja ananena kwa lugha na ndugu fulani anafasiri—Mh.]

135 Mwenyezi! Bwana asifiwe! Sasa, kama unaelewa, rafiki, huyo ni Roho wa Bwana akinena. Sasa, Biblia ilisema, “Mmoja akinena, mwingine anafasiri.” Sasa, Bwana alisema alikuwa tayari kuyafunua macho yenu na kujionyesha Mwenyewe kwenu. Loo, ni ajabu jinsi gani! Hivi hamna furaha kwa ajili yake? Ajabu.

136 Ni kadi gani za maombi zilizotolewa? G. Mwanangu alisema walitoa kadi hamsini za maombi: G, moja hadi hamsini. Tutaziita kadi hizo, muda kidogo tu. Na sasa, kwa kawaida, kwa siku chache zilizopita usiku, hatujakuwa tukigawa kadi za maombi, tumekuwa tukifanya upambanuzi, watu tu wakiomba. Mnapenda hilo? Loo, na—napenda tu jambo hilo. Lakini watu

wengi wanataka kuwekewa mikono, nasi tuko papa hapa kufanya hivyo. Naam, bwana.

137 Sasa, G namba moja, ni nani aliye nayo? Kadi ya maombi namba moja. Sasa. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kama Yeye ni Kuhani Mkuu, na je, Biblia inasema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele"? Unaamini hilo, dada mpendwa? Vema. Unaamini ya kwamba Yeye yuko? Unaamini, maskini mama, uliyeketi hapa kitini? Unaamini ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu? Sawa. Sasa, Yeye anaweza kuguswa na mambo ya udhaifu we—wetu.

138 Kama ningeweza, watu wangu wa thamani, kama ningeweza, ningeshuka moja kwa moja hapo na kuzunguka kote jengoni na kumponya kila mtu hapa. Ni—ningependa tu kufanya hivyo. Ninaamini mnaamini hilo. Ningefanya hivyo, lakini siwezi, siwezi kulifanya, tayari limefanywa, Yesu amefanya hivyo. Hawezi kusamehe dhambi zako, tayari amezisamehe. Lakini sasa, haitakufaa kitu mpaka uukubali, uuamini, unasema, "Naam, Bwana, ninakubali yale uliyonifanyia," ndipo umeokoka.

139 Halafu useme, "Ninataka uniponye, Bwana." Tayari amefanya hivyo, basi inakubidi tu kukubali yale Yeye amefanya. Sasa, Yeye ni Kuhani Mkuu, aliyeketi mkono wa kuume wa Mwenyezi Mungu, akifanya maombezi tunapokiri, ama kuungama, ni neno lile lile. Kwa hiyo, chochote. . .

140 Sasa, Yeye hawezi kutufanyia lolote mpaka tayari tumesema ya kwamba amefanya jambo hilo. Hatuna budi kukiri jambo hilo, ama kuungama, kwamba Yeye amelifanya, ndipo Yeye anaweza kwenda kulitekeleza na kufanya maombezi. Hiyo ni kweli, ndugu? Je, hayo ni Maandiko? Kufanya maombezi tunapoungama.

141 Sasa, nayo Biblia ilisema, katika Kitabu cha Waebrania, sasa, tuna baadhi ya wasomi walio bora sana ulimwenguni usiku wa leo, walioketi hapa, katika Kitabu cha Waebrania, kwamba imeandikwa ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu sasa, aishiye daima, kufanya maombezi tunapoungama, na Yeye pia ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Yeye. . . Tunaweza kumgusa kwa udhaifu wetu.

142 Basi, kama Yeye ni Kuhani Mkuu, na ndivyo alivyo, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, basi, kama Yeye ni yeye yule. . . Waebrania 13:8 ilisema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

143 Sasa, Naye akasema, "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya." Sasa, Yeye alifanya kazi gani kuwafanya watu waelewe ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi? Mnaona? Kwa sababu aliwaonyesha ishara ya nabii, ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi. Walijua jambo hilo, maana Musa alisema ya kwamba Yeye angekuwa ni Nabii. Ni wangapi wanaelewa hilo?

144 Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yesu alisema katika Yohana Mtakatifu 5:19, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda"? Basi Yesu Mwenyewe, Neno hilo ni kweli, Yeye kamwe hakufanya mwujiza mmoja mpaka Mungu alipomwonyesha ono juu ya jambo la kufanya. Vipi kuhusu hilo? Hiyo ni kweli, ono juu ya jambo la kufanya.

145 Nena kuhusu maono! Ndugu huyu, mfasiri hapa, alikuwa akiniambia leo ya kwamba yapata asilimia arobaini ya Biblia ni maono. Nasi tunaninii tu . . . Kama alivyosema, alitoa kielelezo kizuri, kasema, "Hebu bandika mkono wako wala usiutumie kwa miezi kadhaa, na uone kinachotukia. Unakuwa dhaifu sana kiasi kwamba hauwezi kutumika."

146 Hivyo ndivyo kanisa limefanya na mambo haya, pamoja na karama zote za Mungu, mnazibandika tu, haziwezi kutumika. Mnaona? Ziachilieni. Tumieni imani, zitie misuli. Hebu niwaambie, imani ina nywele kifuani. Imani inaponena, kila kitu kingine kinaketi chini. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Inaponena, kila kitu kingine kinanyamaza.

147 Sasa, kama Yesu ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, basi wazieni, ninyi mlio huko nje msio na kadi ya maombi, mnaamini mngeweza kugusa vazi Lake usiku wa leo? Mnaamini mngeweza?

148 Sasa, kama ukipagawa sana, na kusema, "Loo, mimi . . . Hebu—hebu niharakishe, hebu nijaribu." La, utaipoteza papo hapo. Unaona? Imani ni rahisi sana, hujui unayo. Hiyo ni kweli. Ni zawadi tu. Ni kusema tu, "Vema, hivi unaweza kuigusa Biblia hiyo?"

"Hakika."

"Unajuaje unaweza?"

"Ni kwa imani tu, kwa sababu imekuwa tu ni kawaida sana kwangu, ninanyosha tu mkono na kuichukua."

149 Vema, hivyo ndivyo imani ilivyo, ni rahisi sana, unanyosha tu mkono na kuichukua. Sasa wewe amini.

150 Ninyi nyote ni wageni. Ni wangapi katika mstari huu wa maombi ambao ni wageni? Inueni mikono yenu, ninyi tusiofahamiana, ninamaanisha. Vema. Ni wangapi huko nje ambao hatufahamiani? Inueni mikono yenu.

151 Sasa, hatuko kwenye ubao fulani wa uaguzi, kama ibilisi. Tuko hapa nje mbele ya taa hizi na mbele za watu, Uweponi mwa Mungu kumwomba Mungu afanye yale aliyosema angefanya. Sasa, mstari huu hapa si mstari wa upambanuzi. Tunajua tunawaombea tu watu hawa. Upambanuzi huja kutoka huko nje. Mnaona? Watu hawa . . . kama . . . Ni wangapi wanaojua hilo wakati ungeninii . . . ?

[Dada mmoja anatabiri—Mh.] Amina.

152 Aminini. Kwa utamu, aminini. Sasa ninii tu, ninawatakeni ninyi kwenye mstari wa maombi, sasa, angalieni kusanyiko. Mnaona? Nanyi ombeni, na mumwombe tu Baba, “Baba Mungu, Wewe wajua haja yangu, Nawe unajua ya kwamba ninahitaji uponyaji. Utanisaidia?” Kwa unyenyekevu tu, njoo tu kama maskini mwanamke yule aliyekuwa anatokwa na damu, naye akaugusa upindo wa vazi Lake akawa mzima.

153 Hapa pembeni, hivi uliinua mkono wako muda mfupi uliopita? Unataka—unataka kuponywa? Unafikiri moyo wako utakuwa sawa sasa, utaponywa? Ulikuwa na ugonjwa wa moyo, sivyo? Si ulikuwa ukiomba, “Bwana, na iwe ni mimi”? Inua mkono wako kwamba ni kweli. Vema. Ugonjwa wako wa moyo umekwisha sasa.

154 Sasa, simjui huyu mtu, lakini angalieni. Kitu gani? Je, alinigusa mimi? Yuko futi thelathini kutoka kwangu. Mnaona? Aligusa Kitu fulani, na Kitu fulani kikanena kupitia kwangu, hivyo tu. Haikuwa ni mimi. Mimi ni kama tu. . .Maikrofoni hii hapa ni bubu kabisa bila ya kuwa na kitu cha kuzungumza kupitia kwayo, na hivyo ndivyo tulivyo. Ninamjuaje mtu huyo? Kamwe sikujua kile. . .Ningejuaje shida yake? Sijui.

155 Hapa, ili mweze kujua tena, huyu hapa mtu ameketi papa hapa nyuma, akiugua ugonjwa wa moyo, amevaa koti dogo, linaloonekana la samawati huku shati lake likiwa wazi. Hiyo ni kweli, sivyo, bwana? Vema. Alikuponya papo hapo. Imani yako ilikuponya. Unaona?

156 Alifanya nini? Yeye alimgusa, si mimi, simjui huyo mtu, sijawahi kumwona, lakini alikuwa na hitaji sana, naye alikuwa akiomba, “Ee Bwana, jalia Ndugu Branham anene nami.” Mwulizeni kama hiyo ni kweli ama si kweli. Inua mkono wako kama hiyo ni kweli, bwana. Inua mkono wako kama ulikuwa umeketi pale ukiniombea. . .?. . .Unaona?

157 Sasa, Mungu anayeweza kusikia maombi, anaweza kujibu maombi. Hivi hamwoni hivyo?

158 Mama huyu, aliyeketi papa hapa nyuma, ana tatizo na mikono yake. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, mama, ukiwa na tatizo mkononi mwako, uliyeketi hapo? Unataka kuponywa? Vema. Imani yako ilimgusa basi, mikono yako itapona.

159 Mama huyo aliyeketi moja kwa moja nyuma yako hapo, amefanyiwa upasuaji mbaya sana, naye anaomba, pia, apate kumalizana na hilo. Hiyo ni kweli, mama? Inua mkono wako. Vema. Utapona. Mahali ambapo madaktari wanashindwa. . . Shetani alijificha kutoka kwa madaktari, bali hawezi kujificha kutoka kwa Mungu, Yeye anajua papo hapo alipo, kwa hiyo ameondoka. Mwamini Mungu.

160 Mama huyu aliyeketi papa hapa karibu na mahali ambapo mtoto huyo mchanga anapembezwa huku na huku, anauombea

ugonjwa wa mguu. Lakini unaamini ya kwamba Mungu ataiponya hiyo miguu? Kama unaamini, vema, simama, mama, ili kwamba wajue ni nani ninayenena habari zake. Haya basi, wewe, papo hapo, dada. Mwambie tu Mungu ya kwamba unampenda. Unampenda? Vema, basi unaweza kwenda nyumbani na uwe mzima. Bwana akubariki. Hilo ni zuri sana.

161 Na jambo lingine, ulipoketi chini, mama huyo papo hapo karibu nawe alisisimkwa sana, akiwa na ugonjwa huo wa kibofu, lakini umetoweka, pia, dada. Simama tu kwa miguu yako na uukubali, pia. Kwa hiyo, umeponywa.

162 Unaamini kwa moyo wako wote? Sasa, mnaona, sasa tunajua Uwepo Wake upo hapa. Sasa iweni na kicho. Sasa, kama . . .

163 Mtu yeyote anajua kwamba ono linapoingia, linakudhoofisha. Ni wangapi wanaojua hilo? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Mwana wa Mungu alisema, wakati mwanamke alipogusa vazi Lake, alisema, "Ni nani aliyenigusa?" ndipo akaangalia kote, akasema, "Naona kwamba nguvu," huo ni uweza, zimemtoka. Na hilo linahitaji uweza. Vipi, hivi watu hawa wote hapa . . .? Kama Mwana wa Mungu, mwanamke mmoja akimgusa, na kuna watu saba ama wanane upande ule mwingine, basi . . . Mnaona? Nanyi mngali mnagusa, kama nikizungumza tu, mnaona. Ni—ni imani yenu.

164 Lakini sasa, mstari huu hapa, aminini. Sasa, Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

165 Angalia, hivi majuzi usiku, nikipitia huku, nilimwekea mikono mvulana mdogo, kipofu, nikatoka moja kwa moja pale na kuanza kushuka kwenye vipandio, naye akafunguliwa macho. Ni wangapi waliokuwa hapa wakati jambo hilo lilipotukia? Hakika. Mvulana mdogo, aliyezaliwa kipofu, yapata umri wa miaka kumi na sita, kumi na saba. Akaanza kupaza sauti, "Loo, Ndugu Branham, ninaweza kuona!" Hakika. Siwezi kuponya, ninaweza tu kutii amri. Mnaona? Hivyo ndivyo ninavyofanya hapa. Wakati aliponiambia ya kwamba mambo haya yangetukia . . .

166 Na hebu niwaambieni jambo fulani sasa. Ile huduma mpya inayokuja, itakuwa mbali sana na hii, hata . . . Ni . . . Tayari nimeiona ikifanya kazi mara nne ama tano. Kuna wengi wa watu walio pamoja nami wanaojua hilo kuwa ni kweli. Tuko tayari kwa saa kuu.

167 Lakini ili mpate kujua: Huyu hapa mtu mzuri amesimama hapa. Hatufahamiani, sivyo, mama, mimi na wewe? Vema, Yeye haninii . . . Lakini, sina fununu . . . huyu mwanamke. Mimi . . . Ulisema jambo fulani, dada, sikuninii . . . Loo, nilikuombea hapo awali. Uh-huh. Bila shaka, nisingejua hilo. Jamani! Sijui una shida gani sasa. Mungu . . . Ama kama mimi . . . Mungu anajua ya kwamba sikukumbuki, unaona. Lakini ili kwamba tu watu

wapate kuona ya kwamba Mungu ni mkuu vile vile hapa, huko nje. . . Ni popote tu ilipo imani yako.

168 Sasa hivi, ili tu kutulia, mnaona, ninajaribu kujiondoa kwenu, kuzuia imani yenu isivutie huku. Na muda si muda mwajua, ningedhoofika tu kabisa, kamwe huwezi kusimama kupita kiasi. Umwombee mtu fulani, kisha ugeuke, ubadilishe huyo mgonjwa, kisha umwombee mtu mwingine tena upate tu kuimarisha nguvu, kutimiza ahadi yangu ya kuwawekea mikono Wamarekani.

169 Haitubidi kufanya hivyo nchi za ng'ambo, jambo moja tu likitamkwa namna hiyo, kundi zima linasimama tu, wanaacha viti vya magurudumu, na kadhalika, na kwenda nyumbani, yote yamekwisha. Mnaona?

170 Lakini kuna machafuko mengi sana ya mafundisho mbalimbali hapa Marekani, hawajui la kuamini. Hiyo ni kweli. Mmoja anasema, "Loo, telepathia." Mwingine, "Ibilisi." Mmoja anasema, "Fanya *hivi*." Mmoja. . . Maskini enyi watu, sikilizeni, ninyi. . . "Neno la kila mtu na liwe uongo na la Mungu liwe kweli." Hiyo ndiyo njia pekee ya kulisema. Yeye yupo hapa, tayari amekuponya, wewe likubali tu.

171 Sasa angalia, mama, kama Bwana Yesu atanifunulia jambo fulani kukuhusu, ambalo, unajua sijui lolote kukuhusu, na kama Bwana Yesu atanifunulia jambo fulani, ambalo unajua halina budi kuja kwa njia ya kimbinguni, i—ingekufanya uamini vizuri zaidi? Ingekufanya?

172 Je, ingelifanya kusanyiko liamini vizuri zaidi? Sasa, yeye yuko karibu nami, hapa, mnaona, karibu sana.

173 Sasa, hii ni picha ile ile ya Yohana Mtakatifu 4, mwanamume na mwanamke wakikutana kwa mara ya kwanza, wameketi hapa, ninii tu. . . Labda kile kisima kidogo kilikuwa ni mandhari kama hii. Sasa, Yesu akaanza kuzungumza naye. Sasa, wewe siye yule mwanamke, nami si Yeye, bali Roho Wake angali anaishi, unaona. Katika wakati huo, alikuwa katika mwili ulioitwa Mwana wa Mungu, na sasa tumefanywa wana wa Mungu wenye mamlaka, kwa neema Yake, kusudi kazi Zake ziweze kuendelea, unaona, na zingali zinamtangaza Yeye.

174 Mama huyo ni mgonjwa sana, sana. Ana shida ya kike, shida ya akina mama. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

175 Unaamini sasa?

176 Ninaendelea kumhisi mtu fulani akisema, "Anabahatisha hilo."

177 Acha kuwazia hilo, unadhuru mkutano. Sibahatishi hilo, hizo ni nguvu za Mungu.

178 Hapa, simama kimya kwa dakika moja. Angalia sasa, kusudi tu tutoe hilo akilini mwao. Hebu tuone, sijui ilikuwa

ni nini, lakini hebu dakika moja tu mpaka nitakapoipata. Naam, umekuwa kwa da—daktari. Ni wa kike . . . Naam, isitoshe, unapaswa kufanyiwa upasuaji. Hiyo ni kweli. Nawe una shida ya figo, una shida ya kibofu. Hutoki katika nchi hii, unatoka Missouri, jina lako ni Bi. Hildreth. Sasa, rudi kule juu na uwe—na upate afya . . .?. . . amini. Mungu akubariki, dada. Imani yako imekuponya. Amini tu kwa moyo wako wote . . .?. . .

179 Unaamini sasa unapokuja? Nisiposema jambo moja, utaamini kama nikiwawekea wagonjwa mikono? Ninyi wengine mtaamini sasa? Njoo moja kwa moja.

180 Kila mtu awaombee watu hawa sasa.

181 Baba uliye Mbinguni, jalia nguvu za Mwenyezi Mungu zikae juu ya mwanamke huyu, na kumponya. Amina.

182 Vema, njoo. Unaamini, dada? Vipi kama ningekwambia, uliponywa ulipokuwa umeketi kitini wakati Hiyo ilipokuja juu yako? Imeondoka . . .?. . .

183 Unaamini sasa, dada? Kanisa hili lote linakuombea.

184 Baba yetu wa Mbinguni, ninamwekea mikono na kuombea uponyaji wake, katika Jina la Yesu. Amina.

185 Njoo. Sasa, unajua ya kwamba ninajua shida yako. Lakini nisiposema lolote, ungeamini, kwa vyovyote vile? Basi nenda ukale chakula chako cha jioni, ugonjwa wako wa tumbo ulikuacha, unaweza kwenda ule . . .?. . .

Unaamini, dada?

Katika Jina la Bwana Yesu, jalia aponywe.

186 Njoo, bwana. Unaamini ugonjwa wa moyo ulikuacha ulipopanda vipandio dakika chache zilizopita? Kama ningekwambia ulikuacha, ungeamini? Nenda zako, useme tu, "Asante, Bwana Yesu."

187 Njoo huku. Amini kwa moyo wako wote, dada, na hiyo yabisi kavu itaondoka, nawe utakuwa mzima.

Bwana, ninaomba ya kwamba utalijalia, katika Jina la Yesu. Amina.

188 Njoo, dada. Sasa, mimi . . . Unajua ninajua shida yako, sivyo? Unataka nikwambie? Ninaamini unataka. Vema. Sasa, wewe ni mchanga sana kwa huo, lakini una wasiwasi. Sasa, hiyo ni kweli, wasiwasi wa akili, fadhaa, nawe unadhoofika sana karibu mwisho wa alasiri na kuangusha vitu, hivyo ndivyo unavyofanya hasa. Una akili inayowazia, daima unavuka madaraja kabla hujayafikia. Sahau, nenda nyumbani, Yesu Kristo anakuponya. Amini kwa moyo wako wote.

Njoo.

189 Baba Mungu, katika Jina la Bwana Yesu, ninaomba ya kwamba utamponya na kumpa afya mwanamke huyu. Amina.

Endelea . . .?. . .

Baba, ninaomba ya kwamba, katika Jina la Yesu ya kwamba utaponya . . .?. . .

Utaamini sasa, dada, kwa ajili yake?

190 Njoo, mwanangu . . .?. . . Usiwe na shaka. Utaamini kwa ajili yake kwa moyo wako wote, dada?

191 Baba yetu wa Mbinguni, uliwachukua wale wavulana wadogo na kuwawekea mikono, nao wakaponywa. Ninafanya hivi katika, Jina la Yesu. Amina.

192 Amini sasa. Roho Mtakatifu yupo hapa, Roho Mtakatifu yeye yule anayejua yote kuhusu mambo. Sasa, usipotilia shaka hata kidogo, atapona, na awe mzima. Kwa hiyo nenda tu ukiamini. Mnaona?

193 Sasa, ninyi watu mnaopitia, wakati mna . . . mnajua, mnaendelea kuwazia, mnaendelea kushangaa, kuangalia, mwone kama nitawaambia. Kama mimi . . . Watakuja kunichukua na kunitoa mstarini, hao wengine hawatapitia mstarini, mnaona, kwa hiyo msifanye hivyo. Mnaona, Yeye angali hapa. Yeye anajua—Yeye anajua yote kuihusu, anajua kila kitu. Hivi hamwamini hilo?

194 Unaamini hilo, mama? Je, hatufahamiani? Mungu anatujua sote wawili sivyo? Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni ipi? Kama atafanya hivyo kwa ajili ya mwanamke huyu, je, ninyi wengine mtaamini kwa moyo wenu wote usiku kucha? Inueni mikono yenu kama mnasema mtafanya hivyo. Hii hapa mikono yangu, simjui huyo mwanamke, sijawahi kumwona. Vema. Aminini tu.

195 Una mbavu zilizovunjika, hiyo ni kweli, ndiyo shida yako. Kweli kabisa. Una mzigo moyoni mwako kwa ajili ya mtu mwingine unayemwombea. Huyo ni baba mkwe wako, hiyo ni kweli, naye ni kipofu, ana kansa ya tumbo. Utajali kama nikisema hayo mengine? Alikuwa maskini sana asingeweza kuja mkutanoni, hakuwa na pesa za kuja mkutanoni. *Hapa*, weka hiyo juu yake katika Jina la Bwana, chukua leso yangu, na umwambie atapona . . .?. . .

[Ndugu Branham anawaombea wale walio kwenye mstari wa maombi, mengi ya maneno yake hayatambuliki—Mh.]

Katika Jina la Yesu Kristo . . .?. . .

Baba, mimi . . .?. . .

196 Wasiwasi ulisababisha hilo, ukafanya kitu kama kidonda cha tumbo, ukasababisha asidi hiyo kinywani mwako, na kadhalika, baada ya kula. Nenda ukajinunulie sambusa, imani yako inakuponya . . .?. . .

197 Baba yetu wa Mbinguni, ninamwombea mvulana huyu kwamba nguvu za Mungu zitamponya. Amina.

198 Nawe unapita chini ya msalaba kwa ajili yake, amini kwa moyo wako wote. Mungu akubariki, bwana. Amini.

199 Unawazia nini juu ya huyo mtoto mchanga? Wewe, huyo ndiye unayetaka aombewe. Unaamini Mungu angeweza—angeweza kuniambia kuna nini? Ingekusaidia? Ninaona ni jambo zito. Ni ugonjwa wa ubongo, kitu kama mtu kudumaa kiakili. Amefanyiwa upasuaji mara tatu bila kufanikiwa. Unaamini Mungu anaweza kusikia maombi yangu?

200 Basi ninautoa huu uovu . . .?. . .

201 Usitie shaka, atapona . . .?. . .

Bwana, ninaomba ya kwamba utamponya mwanamke huyu, katika Jina la Yesu . . .?. . .

Njoo ukiamini . . .?. . .

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

Ee Mungu, naomba . . .?. . .

Njoo, dada mpendwa . . .?. . .

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

Usiwe na shaka. Nenda, ukiamini.

Njoo kana kwamba unakuja msalabani . . .?. . .

Nenda—nenda ukiamini kwa yote yaliyo ndani yako, sasa . . .?. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

202 Jambo fulani lilitukia kwenye kusanyiko. Mtu fulani aliponywa kwenye kusanyiko. Hebu kidogo, nitalipata.

203 Je, wewe ndiwe wa kuombewa? Unamwamini Mungu? Kuna shida kwenye mapafu yako, una shida katika mapafu yako. Ndio kwanza ushikwe na msongo wa mawazo. Wewe hutoki hapa, unatoka California. Wewe ni mhudumu, Bw. Alsup. Nenda nyumbani, uwe mzima. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Ee Bwana, njoo, naomba, katika Jina la Yesu, ya kwamba utatujalia, Bwana . . .?. . .

Njoo, dada mpendwa.

204 Kila mtu aombe sasa. Ni udhaifu. Ombeni, ombeni, ombeni.

Katika Jina la Yesu ninaomba, Baba, ya kwamba utamponya.

205 Njoo, bwana. Amini kwa moyo wako wote na unaweza kuondoa baragumu yako, katika Jina la Yesu Kristo. Naam, najua unao, najua unao. Amini sasa.

Huyu mvulana mdogo aliyelemaa?

206 Ee Bwana, ninaomba ya kwamba utamponya huyo mvulana mdogo. Jalia arudi, akitembea na kushangilia, katika Jina la Yesu. Amina.

Usitie shaka, sasa. Amini kwa moyo wako wote. Unaona?

Vema. Njoo dada, mpendwa. Amini kwa yote yaliyo ndani yako.

Katika Jina la Bwana Yesu, jalia aponywe. Amina.

Njoo ndugu, kwa imani yote uwezayo, amini.

Katika Jina la Yesu Kristo, naomba uponywe. Amina. Amina.

Njoo, mama.

Ee Baba Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

207 Ombeni, kanisa lote, ombeni pamoja sasa. Ninii tu, vipi kama hawa ni watoto wako wanaopitia hapa?

Njoo . . .?. . .

Ee Mungu, ninaomba ya kwamba utamponya huyu mvulana mdogo na kumpa afya, katika Jina la Yesu. Amina . . .?. . .

Njoo, bwana.

Bwana, katika Jina la Yesu Kristo, mjalie Baba haja yake. Amina.

Njoo, bwana.

Baba wa Mbinguni, jalia ombi hili, na jalia aponywe kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina.

Mungu akubariki, dada, usiwe na shaka . . .?. . . Mungu akubariki . . .?. . .

Baba Mungu, ninaomba ya kwamba utamjalia haja yake anayoombea. Katika Jina la Yesu Kristo, na iwe hivyo. Amina.

Njoo sasa, ukiamini kwa moyo wako wote. Je, unaamini kwa moyo wako wote? Njoo hapa kwa dakika moja tu.

Ee Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba, katika Jina la Kristo ya kwamba utatujalia haja hii, na jalia aponywe kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Amina.

Katika Jina la Yesu Kristo na aponywe, Baba, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Amina.

Angalia ni watu wangapi wanaokuombea huko nje, baba. Huna budi kufanikiwa, huna budi kufanya hivyo.

Baba Mungu, katika Jina la Yesu Kristo mjalie uponyaji kwa ajili ya utukufu Wako. Tujalie.

208 Unaamini kwa ajili ya huyu mtoto? Mleteni hapa.

209 Ee Mungu . . .

210 Usiwe na shaka tena, unaona. Hebu . . . U—ujaribu, bali usifanye hivyo.

211 Baba, na alaaniwe ibilisi ambaye ametenda uovu huu. Jalia mtoto huyo apone.

212 Unaamini ya kwamba Mungu alisikia hilo? Nakwambia, nipate kuwa na hakika ya kwamba utajua, weka kamba

kichwani mwake, halafu ukipime usiku wa leo, ukate hiyo kamba, halafu kesho asubuhi, ama, kesho usiku kabla hujarudi, ukipime tena, halafu basi unionyeshe kimepungua kiasi gani, uiweke hapa dawatini. Ndipo uangalie jinsi kimepunguka kati ya sasa na kesho . . . ?. . . Amini.

213 Utaamini, ukilala hapo? Mtaamini, ninyi nyote? Iweni na imani sasa, ni chochote mnachoamini.

214 Sasa, je, wewe ni . . . ndiwe wa kuombewa? Unamwamini Bwana Yesu? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake? Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? *Nabii* huwafadhaisha watu, mnaona, najua mahali fulani wanaponisikiliza. Dhaifu sana, lakini unaamini ya kwamba Mungu atasikia maombi? Vema.

215 Sikiliza, shida yako iko ubavuni mwako. Hiyo ni kweli. Una mpendwa unayemwombea, na mpendwa huyo kwa namna fulani ana ugonjwa wa akili. Hiyo ni kweli. Unaamini watapata afya? Unaamini leso hiyo uliyo nayo itaushika? Bibi Hammer, hilo ndilo jina lako. Wewe hutoki hapa, unatoka Oklahoma, Wagoner. Sasa, rudi na uchukue leso hiyo. Amini kwa moyo wako wote, na Yesu . . . ?. . .

216 Mnaamini, huko nje, kwa moyo wenu wote, kila mmoja wenu? Mnaamini, kila mtu? Nitawaambieni la kufanya, mkiweza: Nyosha mkono na kumwekea mikono mtu fulani, umwekee mikono. Kijana, weka mikono yako juu ya huyo mtoto, utafanya hivyo? Omba . . . Hiyo ni kweli, weka mikono yako papo hapo juu ya maskini msichana huyo. Vema. Mtu fulani aende pale na kumwekea mikono mama huyu kwenye kitanda cha wagonjwa. Ninyi nyote, ninyi ni waaminio? Semeni, "Amina."

217 Njoni hapa, ndugu, chukueni moja ya maikrofoni hizi, kila mmoja wenu.

218 Inamisheni vichwa vyenu. Yesu Kristo Mwana wa Mungu, Ambaye yupo sasa, anaijua mioyo yenu. Mimi ni dhaifu sana ni vigumu kustahimili sasa; mnaweza kutambua hali hiyo. Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Kama wewe ni mwaminio, mwekee mtu fulani mikono yako, mwombee, nao watakuombea. Sasa, nitawaombea ninyi nyote, na Mungu atayasikia maombi yangu, Mungu atayasikia maombi yako, na sijali una shida gani, wewe amini tu sasa hivi nawe utapata afya, kila mtu.

219 Msichana mdogo aliyelemaa, aliyeketi kwenye kiti cha magurudumu amesimama, katika Jina la Bwana.

220 Sasa, Bwana, ninaomba ya kwamba nguvu Zako na neema zitatosha wakati huu katika mioyo ya watu, kama yule malkia wa Sheba, jalia wasimame leo, wakithibitisha Mungu yuko katikati ya watu Wake.

221 Shetani, wewe uliyewafunga watu hawa, nakuapisha wewe kama mdanganyifu, nakuapisha kwamba huna mamlaka, wewe ni mdanganyifu tu. Yesu Kristo alishinda nguvu zote ulizo nazo, na kukuvua kila mamlaka. Unawadanganya watu, nawe umefichuliwa usiku wa leo. Toka kwenye kusanyiko hili, katika Jina la Yesu Kristo, waache hawa watu!

60-0401E Malkia Wa Sheba
Municipal Auditorium
Tulsa, Oklahoma Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org